

Uchanganuzi Wa Umilisi Wa Kiisimu Wa Wanafunzi Wa Lugha Ya Kiswahili Katika Chuo Kikuu Cha

Kimataifa Metropolitan

Nuwagaba Medad¹, Mukoyani Geofrey²

Dhahania

Katika chuo kikuu kikuu kimataifa cha Metropolitan kumekuwa na tatizo kubwa la umilisi mdogo wa kisimu kwa wanafunzi wanaofunga masomo ya Lugha ya Kiswahili. Hii imekuwa kwa kipindi cha miaka mingi sasa bila kupata ufumbuzi wa kudumu. Utafiti huu unategemea kufanya uchambuzi kamili kwa kutumia mbinu mbalimbali za utafiti ili kujua sababu za kina za tatizo hili na kupanga mikakati sahihi ya kulilia tatizo hilo. Matokeo yenyewe yatafananishwa na matokeo ya vifaa vya utafiti waliopita katika changamoto hii. Katika utafiti huu utafiti atatumia michango ya wanafunzi, walimu na viongozi wa chuo kuu katika ngazi mbalimbali kwa njia ya mahoiano maalum, maswali, makaratasi ya maoni na kambi za kujadili. Pia uta analizi wa takwimu za kisayansi kutoka katika rekodi za chuo kuu zikiwemo matokeo ya mihani, idadi ya wanafunzi, ukubwa wa programu na uelekeo wa mafanikio ya wanafunzi kwa miaka. Hivi ni mbinu madhubuti zitakazomsaidia kupata ufumbuzi na tafsiri sahihi za tatizo hili la muda mrefu limeshambaa.

Maneno Muhimu: Uchanganuzi, Wanafunzi, Lugha ya Kiswahili, Utafiti and Mikakati

Usuli wa Mada

Ufundishaji wa isimu kwa Kiswahili umezongwa na matumizi ya istilahi mbalimbali zinazotumiwa na wataalam katika ujifunzaji na ufunzaji wa isimu. Hali hii huenda inapinga kunawiri kwa kozi hizi za isimu na kuathiri kiwango cha ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Tafiti zimedhihirisha kuwa wanafunzi hutofautiana katika umilisi wa stadi za kiisimu. Hata hivyo kazi hizi zinakosa uangavu wa kutosha wa kuchanganua umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa vyuo vikuu, changamoto na athari za kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa misingi hii kunahitajika utafiti bayana unaotambulisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile kuchambua katika kitengo finyu zaidi makosa ya kiisimu na namna makosa haya yanaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Mtalaam Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za lugha na vile vile katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile. Hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano. Umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano. Hata hivyo pana haja ya kutafiti na kutambua makosa ya kiisimu na namna makosa hayo yanathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ili kuweza kupendekeza njia ambazo wahadhiri wanaweza kutumia kuimarisha umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Uganda. Mtalaam Buliba (1998) anaeleza kuwa wahadhiri wa isimu katika Kiswahili hukumbana na matatizo katika ufunzaji wa somo hili katika vyuo vikuu. Anaeleza kuwa changamoto za

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

istilahi tofauti huwakanganya wanafunzi na kufanya umilisi wao wa isimu katika Kiswahili kuwa wa kiwango cha chini. Naye Mathooko (2000), anaongezea kwa kusema kuwa, dhana nyingi na tofauti za kiisimu katika lugha ya Kiswahili hutokana na tafsiri za Kiingereza ambazo hutumiwa na wahadhiri wakati wa ufunzaji wa somo la isimu katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na Chomsky (1965) Viwango vya umilisi katika lugha yoyote ile huweza kukadiriwa kwa namna nyingi. alizua dhana ya umilisi wa lugha. Umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile: Kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha ipasavyo.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Richard na Rodgers (1986) wanaosema kuwa mtu kuwa na kiwango fulani cha lugha sio lazima amiliki sheria za lugha pekee bali aweze kutumia sheria hizo katika utendaji (yaani katika mazungumzo na maandishi). Utafiti huu unafanywa katika eneo la wingi lugha ambapo lugha za kwanza ni nyingi mno. Wanafunzi wanapojiunga na chuo huwa na viwango tofauti vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo viwango hivi tofauti havijulikani bayana na ni vipi viwango hivi huathiri umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Utafiti kuhusu viwango hivi katika Chuo Kikuu utawapa wahadhiri, watalaam wengine na wakuza mitaala habari muhimu ambayo itawawezesha kutafuta njia na mbinu za kuimarisha ufundishaji wa umilisi wa Kiisimu katika uandishi wa kiakademia miongoni mwa wanafunzi wa somo la kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utafanyika katika Chuo Kikuu cha kimataifa cha Metropolitan bewa wa la mbarara wilayani mbarara na hali inayoendelea inapata changamoto kuhusu uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa lugha ya kiswahili katika chuo kikuu cha kimataifa metropolitan. Madhara makubwa ni pamoja na uhaba wa vifaa vya kutumia, uhaba wa kuacha, uharibifu wa mazingira, uhaba wa wadau wa lugha, na usogo wa kukuza na kueneza lugha ya kiswahili. Vipengele hivi husababisha utendaji duni iwe wa moja kwa moja au usio wa. Watu wengi katika eneo hilo hawajasoma na kwa hivyo hawajui umuhimu mkubwa wa kujifunza lugha ya Kiswahili katika eneo lao, yaani, baadhi yao hawajui kusoma na kuandika. Haya yote yamechangiwa na serikali kwa kutoweka sera za kudhibiti lugha ya kiswahili kuwa lugha lazima ili iweze kukua kwa kasi, ili kupunguza idadi ya waathirika wa uhaba wa lugha ambao wanaathiri kizazi kinachokua, ili kupunguza athari hizo kwa hivyo serikali inapaswa kuweka sheria kali na sheria. kanuni za kutumia lugha ya kiswahili, kwa mfano kwa kuwaweka kila shule iwe lazima kuwa na somo la kiswahili.

Suala la utafiti

Utafiti huu unalenga kupendekeza njia ambazo wahadhiri wanaweza kutumia ili kuimarisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu

Malengo Mahsusi

1. Kubainisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan.
2. Kuchunguza athari za Kinyankore kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan.
3. Kufafanua uhusiano kati ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na athari za kinyankore ambazo zinawakumba wanafunzi na wahadhiri wa isimu katika lugha ya Kiswahili katika idara ya Kiswahili na lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan.

MBINU ZA UTAFITI

Uchanganuzi wa data ya utafiti huu utaongozwa na muundo wa kithamano. Data hii inapatikana kutokana na makundi tofauti na mashirika makubwa makubwa (Lee 1994). Muundo huu wa mkingamo unaelezwa na Mtaalam Ilomak (2005), kuwa ni kifaa cha utafiti kinachotumiwa kukusanya habari kutoka kwa washirika wengi kwa wakati mahsusi. Data hii hutokana na washiriki wenye uwezo na tabia tofautitofauti. Muundo huu unamwezesha mtafiti kulinganisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa tatu. Muundo huu unachunguza wahusika kulingana na miaka, jinsia, mapato na viwango vya elimu. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa utatumia uchanganuzi wa kithamani kuchambua vigezo muhimu vya utafiti na kuimarisha matokeo ya data kwa kutumia uchanganuzi wa kiidadi. Muundo huu unafaa utafiti huu kwa sababu unachunguza viwango vya umilisi wa kiisimu, viwango vya kielimu na kijinsi. Eneo la utafiti huu ni Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan nchini Uganda Bewa la Mbarara. Chuo hiki kinapatikana jijini Mbarara katika barabara kuu la masaka – kampala. Hiki ni chuo cha binafsi na hufundisha kozi nyingi, Kiswahili kikiwemo. Utafiti unafanywa katika idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika chuo hiki. Sehemu ya isimu inashughulikiwa ikiwa ni uchanganuzi wa sentensi changamano. Walliman (2011) anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti (vinavyotafitiwa), yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Hivyo, kundi lengwa katika utafiti huu ni wanafunzi wa isimu katika Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika na wahadhiri wanaunda idadi lengwa ya utafiti huu. Wanafunzi wanaoshiriki katika utafiti huu ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wa mwaka wa tatu. Vilevile wahadhiri wanashiriki katika utafiti huu. Walengwa hawa wanachaguliwa kwa sababu ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika katika utafiti huu. Sehemu hii inashughulikia sampuli ya utafiti na namna sampuli hiyo inavyoteuliwa. Kothari (2004) anafafanua sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Utafiti huu unahusisha sampuli ya watafitiwa 50 kutoka kundi nzima la watu 145, kati ya hawa

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

wanafunzi 20 ni wa mwaka wa kwanza ambao ni asilimia 40%, wengine 27 ambao ni asilimia 47%ni wa mwaka wa tatu na asilimia 3% ni wahadhiri kutoka idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ambayo.

Jedwali Na. 1: ya idadi ya sampuli ya watafitiwa

Sampuli	Marudio	Wataaoshiriki	Asilimia
Wanafunzi wa mwaka wa kwanza	75	20	40
Wanafunzi wa mwaka wa tatu	67	27	54
Wahadhiri	04	03	06
Jumla	100	50	100

Asilia: Data ya uwanja Mei 2023

Kwa mujibu wa Sigh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli inachaguliwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na usampulishaji nasibu na usampulishaji usio nasibu.

Ruane (2005) anafafanua usampulishaji nasibu kuwa ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua mhusika yeyote katika kundi lengwa huwa mkubwa. Kwa maneno mengine usampulishaji nasibu ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo kila memba katika kundi lengwa ana fursa sawa ya kuchaguliwa kuingia katika utafiti. Usampulishaji usio nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambao huegemea zaidi maamuzi ya mtafiti na hauwezi kutoa matokeo jumuishi kuhusiana na kundi lengwa. Yaani, ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo sehemu ya watafitiwa huchaguliwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji wao kuliko uwakilishi wao. Wahadhiri watatu wanachaguliwa kwa kuzingatia sampuli hii. Moja kati ya sampuli inayopatikana kwa njia hii ni sampuli ya makusudi. Sampuli ya makusudi ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Mtafiti anaamua kutumia aina hii ya sampuli katika utafiti wake kwa sababu anaamini kuwa kundi hili ndilo lenye uwezo wa kutoa taarifa faafu na wakilishi kwa kundi lengwa katika utafiti. Saunders na Lewis (2003), wanasema kuwa usampulishaji ni njia ya kuchunguza habari kutoka kwa watu wachache ambao watawasilisha idadi kubwa ya watu.

Mtafiti anajumuisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa sababu ndio mwanzo wanajiunga na chuo na ni muhimu kujua viwango vya umilisi wao wa kiisimu katika Kiswahili. Nao wanafunzi wa mwaka wa tatu wanajumuishwa kwa sababu wanaelekea kumaliza mtaala mzima wa kiisimu katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan na hivyo wako katika hali nzuri ya kuelewa kama umilisi wao wa lugha katika Kiswahili unaimarika au la. Mbinu za utafiti zinafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ziko katika makundi makubwa mawili, ambayo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganua data. Data ya msingi inakusanywa kupitia usaili, hojaji na jarabati ya isimu. Vifaa vinavyotumiwa kukusanya data ni: vifaa vya ipod

Received: 17.04.2024**Accepted: 23.04.2024****Published on: 29.04.2024**

kunasa mahojiano baina ya mtafiti na wahojiwa na maswali ya usaili. Tasnifu mbalimbali, mtandao, majarida na makala muhimu kwa utafiti huu. Mtafiti anahitajika kutembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan na vyuo vikuu vingine ili kupata mapitio ya maandishi na kuyanakili kwa kalamu na karatasi. Kuna mahojiano ya ana kwa ana kati ya wasailiwa na msaili. Mahojiano ya wanafunzi yamesadia kuelewa ikiwa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi unaimarika kwa kiwango kipi wanapoendelea kusoma katika chuo hiki. Data inayopatikana inasaidia kuafiki lengo nambari moja na nambari nne, ambapo lengo nambari moja linataka kujua kiwango cha umilisi na lengo nambari tatu linataka kufahamu changamoto wanazokumbana nazo wanafunzi hawa wa isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Metropolitan nchini Uganda. Kulingana na Cohen na Manion (1994), usaili ni mazungumzo ya watu wawili kwa sababu ya kupata data ya utafiti. Naye Weiner (2000) anasema kuwa usaili ni mazungumzo ya ana kwa ana kwa ajili ya kukusanya data kutoka kwa wasailiwa. Katika kuandaa na kushiriki katika usaili mtafiti anatilia maanani umuhimu na udhaifu wa usaili. Katika utafiti huu majibu ya wasailiwa hayaelekezwi na msaili, sampuli ndogo inatoa data inayoridhisha, kujulikana kwa msailiwa haikua shida kwa sababu anatoa data inayohitajika, gharama ya utafiti imepunguzwa kwa kutumia muda mchache katika usaili huu na msaili anajaribu sana kupunguza maswali wazi, ili data inapochanganuliwa isilete utata.

Data katika utafiti huchanganuliwa kwa kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala wa kimaeezo. Kwa mujibu wa Walliman (2011), mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo hutumia namba kurekodi taarifa na huchanganuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu. Naye Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala wa kimaeezo ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti anaeleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Aidha, Kress (2008) anafafanua mkabala huu kuwa unaelezea vipi na kwa nini matukio yanatokea jinsi yalivyo. Kwa kuzingatia umuhimu wa kila mkabala, mtafiti ameamua kuchanganua data za utafiti huu kwa mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Mtafiti anatumia mkabala wa kiidadi kwa lengo la kupata takwimu sahihi za data. Vilevile, mkabala usio wa kiidadi unatumika kwa vile kuna data zinazotokana na majibu ya kimaeezo yanayogusa maoni ya mhojiwa. Kwa hivyo, data hizo zinahitaji kutolewa maelezo. Data zinazopatikana zinawasilishwa kwa kutumia maelezo na jedwali kwa njia ya asilimia. Data katika utafiti huu itachanganuliwa kwa mkabala wa kithamano. Kwa mujibu wa Enon (1998), mkabala wa kithamano ni mbinu ya kuchanganua data ambayo Mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Naye Kress (2008) anafafanua mkabala wa kithamano kuwa unaelezea vipi na kwa nini matukio yametokea. Mkabala huu utatumika kwa vile kutakuwa na data iliyotokana na majibu ya kimaeezo yaliyogusa maoni ya wahojiwa. Kwa hivyo, data hiyo itahitaji kutolewa maelezo. Data itakayopatikana itawasilishwa kwa kutumia maelezo na majedwali.

Data itakayokusanywa itapangwa kwa utaratibu ili kuwezesha uchanganuzi kufanywa. Mtafiti atatumia njia ya kitarakimu kuchanganua ile data kisha akaiwasilisha kwa kutumia idadi, asilimia, majedwali pamoja na maelezo ili kuwezesha ile data kueleweka. Uchanganuzi huu utamsaidia Mtafiti kujadili matokeo, kufafanua na hata kutoa

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

mapendekezo kuhusu yale matokeo. Mchakato huu unajumuisha aina mbalimbali za kazi na taratibu, kama vile: Kukusanya, kuchakata, kuthibitisha na kuhifadhi data. Kuunganisha aina tofauti za data kutoka vyanzo tofauti, ikijumuisha data iliyopangwa na isiyo na muundo. Benard (2012) data za msingi ni zile anazozipata mtafiti moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa, utafiti hutumia mbinu kama dodoso, hojaji na mahojiano ya makundi 39 katika kukusanya data (ty). Mtafiti ametumia data za msingi kwa kiasi kikubwa katika utafiti wake. Taarafa hizo zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa lugha ya kiswahili katika chuo kikuu cha kimataifa metropolitan. Data za msingi zilisaidia kukusanya na kupata taarifa sahihi kuhusiana na mada, kama tujuavyo taarifa hizi hazipatikani mpaka mtafiti awatembelee watafitiwa ili aweze kupata taarifa kuhusiana na kile alichopanga kukitafiti. Hivyo mtafiti aliwatembelea watafitiwa ili aweze kupata taarifa kuhusiana na kile alichopanga kukitafiti. Hivyo mtafiti aliwatembelea watafitiwa na kupata taarifa alizotegemea kuzipata kutokana na mada yake.

Matokeo

Jedwali 2 Alama za UACE.

Gredi	mwaka wa1	Asilimia	mwaka wa 4	Asilimia
A	10	10	5	12.5
A-	05	12.5	3	7.5
B+	06	15	6	15
B	06	15	7	17.5
B-	08	20	7	17.5
C+	11	27.5	12	30
Idadi	40	100	40	100

Chanzo; Saili ya mwaka wa kwanza na hojaji ya mwaka wa nne

Kutokana na matokeo haya, watafitiwa 4 wa mwaka kwanza ambayo ni asilimia 10 waliopata alama ya A katika mtihamu wa Kitaifa wa UACE katika somo la Kiswahili. Watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walipata alama ya A-, watafitiwa 6 ambayo ni asilimia 15 walipata alama ya B+ na B, watafitiwa 8 ambayo ni asilimia 20 walipata alama ya B-. Nao watafitiwa 11 ambayo ni asilimia 27.5 walipata alama ya C+. Ukilinganisha na mwaka wa nne,

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walipata alama ya A, watafitiwa 3 ambayo ni asilimia 7.5 walipata alama ya A-, watafitiwa 6 ambayo ni asilimia 15 walipata alama ya B+, watafitiwa 7 ambayo ni asilimia 17.5 walipata alama ya B na B-. Nao watafitiwa 12 ambayo ni asilimia 30 walipata alama ya c+. Kutokana na matokeo haya utafiti umeelewa alama walizopata wana- funzi katika mtihani wa lugha ya Kiswahili na kuwawezesha kujiunga na chuo kikuu. Alama zao hizi zinatoa maelezo kuhusu umilisi wao wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaoji- funza lugha ya Kiswahili. Kujua huku kunamwezesha mtafiti kuelewa ikiwa umilisi un- aimarika au la wanapozidi kusoma. Kwa kutumia mhimili wa Lehmann wa tatu unaosema kuwa umilisi wa mtu katika lugha hupimwa kupitia mtihani maalum. Hivyo mtihani wa Kiswahili wa kidato cha nne (UACE) unaweza kueleza viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga na Chuo Kikuu kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo juu.

Jedwali la 3. Muhtasari wa matokeo

Wavulana			wasichana	
Alama	marafukizi	Asilimia %	marafukizi	Asilimia
0- 29	3	16.6	2	09
30-34	2	11.1	2	09
35-39	1	5.5	3	13.5
40-44	1	5.5	2	09
45-49	1	5.5	1	4.5
50-54	0	00	5	22.5
55-59	2	11.1	0	00
60-64	4	22.2	3	13.6
65-69	3	16.5	3	13.6
70-74	1	5.5	1	4.5
75-100	0	00	0	00

Idadi	18	100	22	100
--------------	-----------	------------	-----------	------------

Chanzo; Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne.

Kutokana na matokeo haya wavulana 3 ambayo ni asilimia 16.6 walipata alama zisizo zidi 29 ikilinganishwa na wasichana 2 ambayo ni asilimia 9, watafitiwa wavulana 2 ambayo ni

asilimia 11.1 walipata alama zisizozidi 34 ikilinganishwa na wasichana 2 ambayo ni asilimia 9. Mtafitiwa mvulana 1 ambayo ni asilimia 5.5 alipata alama zisizozidi 49 ikilinganishwa na wanafunzi wasichana 2 ambayo ni asilimia 9 waliopata alama sawa na mvulana. Wavulana 9 ambayo ni asilimia 39 walipata alama zisizozidi 69 ikilinganishwa na wasichana 6 ambayo niasilimia 27.2 waliopata alama zisizozidi 69. Hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata zaidi ya alama 75. Matokeo zaidi yanatokana na jarabati ya mwaka wa nne kama yafuatayo; Katika jarabati (kiambatisho 11) mtafitiwa anashindwa kuchanganua sentensi “Nyumba ilijengwa na mwashialiyehitimu” akitumia mstari. Vilevile anashindwa kabisa kuchanganua sentensi nambarimbili “Mtoto aliupiga mpira uliokuwa mweusi”. Kushindwa kwake huku kuchanganua sentensi kunaonesha umilisi wa kiwango cha chini cha kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Majibu ya watafitiwa

Watafitiwa wanaeleza vipengee ambavyo vinaonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vipengee hivi vinapatikana katika utendaji ambapo mtafitiwa anapoandika na kuzungumza mabadiliko haya huonekana. Saili ya watafitiwa wa mwaka wa kwanza nahojaji ya mwaka wa nne inatoa hoja zifuatazo kama vipengee vinavyoonesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu.

Katika mazungumzo vigezo hivi ni:

- i. Miundo mizuri ya sentensi ii. Kuongea kwa ufasaha
- ii. iii. Kutumia sarufi nzuri iv. Kuwa na muwala

v. Kutositasita katika mazungumzo Katika maandishi vigezo hivi ni:

- i. Sarufi nzuri ii. Uakifishaji mzuri wa makala
- iii. Hijai nzuri iv. Miundo ya sentensi v. Nje

Kutokana na matokeo haya vigezo vinavyoonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu vimeorodheshwa. Uundaji mzuri wa sentensi katika mazungumzo, kuongea kwa ufasaha, kutumia sarufi vyema, kuwa na muwala katika mazungumzo yako na kutositasita katika mazungumzo ni vigezo vinavyoonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile Katika maandishi, mtafitiwa ambaye angeandika sentensi vizuri, atumie alama za uakifishaji vizuri, awe na hijai nzuri na atumie nje vizuri anaonesha kuwa umilisi wake wa kiisimu unaimarika.

Mfano mwingine wa matokeo ya mabadiliko ya umilisi yanatokana na wahadhiri ambao wanasema yafuatayo: Mhadhiri A anasema kuwa, *ukimpa mwanafunzi jarabati na kisha uisahihishe unaweza kujua kutokana na alama*

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

anazopata umilisi wake wa kiisimu. Vilevile ukizungumza naye utapata kuelewa jinsi anavyounda sentensi na kupanga mawazo yake kati-ka mazungumzo hayo na utajua kama umilisi wake ni wa kiwango cha wastani, chini au cha juu, pia anapowasilisha kazi yake ya utafiti mbele ya wenzake utafahamu umilisi wake ku- husu lugha ya Kiswahili. Atatumia miundo mizuri ya sentensi, ataongea kwa ufasaha, ata- tumia sarufi nzuri na ataonyesha muwala katika mazungumzo yake. (saili)

Mhadhiri B anaeleza kuwa, vigezo vinavyoonesha badiliko la umilisi katika maandishi, ma- tokeo ni: *Sarufi, njeo, msamiati, hijai na uakifishaji*. Mwanafunzi anapoitumia sarufi vizuri, njeo, msamiati, hijai na uakifishaji unaokubaliwa na wanajamii lugha husika huwa na kiwan-go cha juu cha umilisi wa kiisimu. Naye mhadhiri C anaeleza kuwa, wakati mwanafunzi an- aposoma makala, utaona kuwa *anasitasita, kurudiarudia maneno au sentensi, kuchekacheka na wakati mwingine anashindwa na kunyamaza*. Wahadhiri A, B na C wanaeleza vipengee ambavyo huonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha. Mhadhiri A anaeleza kuwa wanafunzi wakiwa katika mwaka wa kwanza huonesha upungufu katika maandishi yao na vilevile katika mazungumzo yao. Mhadhiri B, anaeleza kuwa sarufi, njeo, msamiati, uaki- fishaji mzuri na miundo mizuri ya sentensi kama vigezo vinavyoonesha mabadiliko haya. Mhadhiri C anaeleza kuwa kusitasita, kurudiarudia katika maneno, kuchekacheka wakati wa kuulizwa maswali na kunyamaza ni vipengee vinavyoonesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu. Mwanafunzi ambaye huonesha haya atachulikwa kuwa na umilisi wa kiwango cha chini. Lakini yule ambaye hataonesha upungufu huu atachukuliwa kuwa ana umilisi wa ki- wango cha juu wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya Lehmann ya umilisi wa kiisimu, vipengee vinavyoonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika utafiti huu ni vile vinavyotumiwa na watafitiwa wengine. Vipengee hivi vinabadilika mtu anavyozidi kukua na kusoma kulingana na mhimili wa lehmann wa pili.

Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili

Lengo la tatu la utafiti huu ni kubainisha maoni ya watafitiwa kuhusu athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa kutumia mbinu ya hojaji na saili, mtafiti amekusanya mawazo mbalimbali ya watafitiwa kuhusu athari za lugha nyingine kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Majibu yanapatikana kutoka swali nambari 6 na 7 (Tazkiambatisho 1, 2 na 3 uk 107-111). Sheng' ilichunguzwa kwa sababu ni msimbo unaotumiwa sana na watafitiwa katika Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan.

Matokeo ya watafitiwa

Kutokana na majibu yanayotolewa na watafitiwa kutoka saili na hojaji ya watafitiwa baada ya uchambuzi wa kina, imebainika kuwa matumizi ya sheng' inaleta athari hasi kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Athari zote ambazo zimetolewa na watafitiwa ni za kiisimu na zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

Athari za Kiisimu

Athari za kiisimu ni athari zote zinazobadilisha vipengele vya lugha na kuvifanya viathirike; kwa mfano, vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na kimsamiati.

Jedwali 4. Athari za Kiisimu Zinazoletwa na sheng' katika Kiswahili

Sampuli ya watafitiwa Athari za kiisimu

Hojaji	A	B	C	D	E
Idadi	4	5	13	9	11
Asilimia	10	12.5	32.5	22.5	27.5
40	4	5	13	9	11

Data kutoka uwandani 2023.

Kifasili

A----- Athari za kifonolojia B----
---- Athari za KimofolojiaC----
---- Athari za Kisintaksia D----
---- Athari za KisemantikiE----
---- Athari za kimsamiati

Athari za Kifonolojia

Athari ya kwanza ambayo imeelezwa na watafitiwa ni ya kifonolojia. Jedwali nambari 4 linaonesha kuwa athari hii ilichaguliwa mara 4 ambayo ni asilimia 10 na watafitiwa. Wa- tafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walichagua athari za kimofolojia. Watafitiwa 13 ambayo ni asilimia 32.5 walichagua athari za Kisintaksia. Watafitiwa 9 ambayo ni asilimia 22.5 wa- lichagua athari za kisemantik na watafitiwa 11 ambayo ni asilimia 27.5 walichagua athari za kimsamiati.

Athari za kifonolojia ni athari zote ambazo zinaathiri matamshi au sauti (fonimu) za lugha mahususi. Katika utafiti huu, watafitiwa wanaeleza kuwa athari kubwa ya kifonolojia ina-yoletwa na mtagusano wa lugha ya Kiswahili na sheng'. Hali hii hubadilisha baadhi ya herufina sauti za Kiswahili. Kubadilisha sauti za Kiswahili ni athari kubwa katika lugha kwani ndizo zinazotofautisha maana. Pia, sauti huunda silabi na silabi ndizo zinazounda maneno ya lugha mahususi. Katika utafiti huu imegundulika kuwa baadhi ya herufi za Kiingereza na lugha za kwanza zinatumiwa kwa

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

ajili ya kuwakilisha herufi na silabi za Kiswahili.

Athari za Kimofolojia

Watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walichagua hii hoja kama inayoathiri umilisi wa kiismukatika Kiswahili kwa watafitiwa wa Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan. Athari za kimofolojia ni athari zote ambazo zinaharibu maumbo ya maneno katika utafiti huu. Watafitiwa wanaeleza kuwa matumizi ya sheng' yanasababisha kuharibika kwa mofolojia (maumbo) ya lugha ya Kiswa- hili. Yaani Kuundwa kwa viambishi na maneno yasiyokubalika katika Kiswahili kutokana na kutofuata utaratibu sahihi wa kuunda maneno kwa baadhi ya mbinu. Athari za kimofolojia ni mbaya sana katika lugha kwa sababu tawi hili ndilo linalohusika na uundaji wa maneno. Hivyo, kama litaathirika maneno yatakayoundwa hayatakubalika katika lugha. Licha ya kuwauundaji wa maneno katika sheng' unatumia mbinu mbalimbali kama vile *finyazo*, *kutohoa na unyambuzi*, maneno yanayoundwa kwa njia hizo aghalabu si sahihi na hayakubaliki katika umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Matokeo mengine yanayotokana na saili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza ni: *Mmekamu kutucheki, doo, beste, buda, fathee nambuyu*.

Saili inaonesha uundaji wa maneno yasiyo ya Kiswahili. Wakati mwingine maneno ya Kiswahili yanaambishwa katika maneno ya Kiingereza na kupewa matamshi ya Kiswahili. Kati- ka maneno haya, “mmekamu kutucheki”, *Kamu* ni neno (come) la Kiingereza lenye maana yaKuja. Katika neno *cheki*, ni kuangalia au hundi katika lugha ya Kiingereza. Vilevile kuna

baadhi ya maneno kama, *doo, beste, buda na fathee* ambayo yanatumiwa na wanafunzi. Matumizi ya neno *doo* kumaanisha pesa, *beshte* kumaanisha rafiki, *buda* kumaanisha baba au tajiri na *fathee* kumaanisha baba linatokana na neno la Kiingereza *father*. Hata hivyo nenohili linafupishwa kwa kudondosha silabi ya mwisho {r} na kuongeza {e}. Neno hili linapewa matamshi ya Kiswahili {fathe}.

Athari za Kisintaksia.

Athari za kisintaksia ni athari zote ambazo zinaharibu muundo wa lugha (mpangilio wa maneno). Watafitiwa wanaeleza kuwa sheng' inaathiri Kiswahili kwa sababu inaharibu sintaksia ya lugha. Yaani, kuharibu muundo wa lugha kutokana na kuchanganya misimbo, kutofuata upatanisho wa kisarufi na kutumia mpangilio wa maneno usio sahihi. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009), sintaksia ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi na mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Watafitiwa wanaeleza kuwa mtindo huu haufuati kanuni za matumizi ya lugha. Hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya sentensi zinachanganya misimbo (Kiingereza na Kiswahili). Kwa mfano,

S “Wasee wakichota tutado zile maswali”

Muhtasari wa tasnifu.

Utafiti huu unachunguza “umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili; changamoto na udhihirifu katika Chuo Kikuu

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

cha Kimataifa metropolitan nchini Uganda. Jumla ya watafitiwa 124 wanashiri- ki katika utafiti huu wakiwemo wanafunzi na wahadhiri kutoka Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan.

Utafiti umelenga kuchunguza mambo manne. Kwanza, kubainisha viwango vya umilisi wa kiisimu kwa wanafunzi wa mwaka kwanza na mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan, Kueleza vipengee vinavyoonyesha mabadiliko la umilisi wa kiisimu katika Lugha ya Kiswahili, kueleza athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kati-ka Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan na kufafanua changamoto ambazo wahadhiri na wanafunzi hukumbana nazo wakati wa kufunza na ujifunzaji katika Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan. Mpangiliomzima wa kazi hii ulikuwa kama ifuatavyo: Sura ya kwanza inatoa taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti. Sura iligawika katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza imeeleza utangulizi wa jumla wa mada ya utafiti. Sehemu ya pili imeeleza suala la utafiti. Sehemu ya tatu imetoa maswali ya utafiti. Sehemu ya nne imeeleza madhumuni ya utafiti. Sehemu ya tano imeeleza umuhimu wa utafiti. Sehemu ya sita imeeleza upeo wa utafiti na sehemu ya mwisho imeeleza misingi ya kinadharia ya utafiti.

Sura ya pili inaeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali juu ya umilisi wa kiisimu wa lugha na nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu. Sura ya tatu nayo imefafanua namna utafiti ulivyofanyika. Sura iligawanywa katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza imeonesha muundo wa utafiti. Sehemu ya pili imefafanua kundi lengwa. Sehemu ya tatu imeeleza eneo la utafiti. Sehemu ya nne imeeleza mchakato wa usampulishaji. Sehemu ya tano imeeleza mbinu za kukusanya na kuchanganua data. Sehemu ya sita imeeleza maadili katika utafiti na sehemu ya saba imeeleza udhabiti wa vifaa vilivyotumika katika utafiti.

Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data ambazo zimekusanywa katika utafiti huu na sura ya tano imetoa muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti. Sura imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza imetoa muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili imetoa matokeo ya utafiti huu. Sehemu ya tatu imeeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne imetoa mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

Muhtasari wa matokeo ya utafiti.

Muhtasari huu umepangwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambyo ni manne.

Katika kuchunguza madhumuni ya kwanza ya utafiti huu, matokeo yanaonesha viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza huwa vya chini lakini wanafunzi wa mwaka wa nne huwa na viwango vya juu vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Sababu ambazo zimetolewa kwa hivi viwango tofauti ni ku- wa, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanapotoka katika shule za upili wanakuwa hawaja- tangamana na kazi za chuo. Lakini wanafunzi wa mwaka wa nne huwa tayari wanamalizia mtaala wa isimu katika Chuo Kikuu na hali hiyo inachangia umilisi wao kuwa wa kiwango cha juu.

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

Matokeo ya jarabati ya wanafunzi wa mwaka wa nne yameonesha kuwa umilisi wa wana- funzi ulikuwa wa juu ingawa kuna wale ambao wanaonesha makosa ya kurudiarudia katika sentensi na wengine wanashindwa kumaliza kujibu maswali. Wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi wanapata alama 33 kwa 40 ambayo ni asilimia 82.5, na wale wa chini wanapata alama 14 ambayo ni asilimia 35. Vilevile viwango vya umilisi wa wanafunzi wa kike vimeonekana kuwa vya juu kuliko wenzao wa kiume. Utafiti umebaini kuwa kuna vigezo tofauti vya kupima umilisi wa kiisimu katika lugha. Vigezo hivi ni jarabati ya maandishi na jarabati ya mazungumzo. Vigezo vingine ni uchunguzi, usikilizaji na usomaji. Hata hivyo utafiti huu uli-tumia vigezo vya kuzungumza na kuandika.

Matokeo ya swali hili yameonesha kuwa badiliko la umilisi wa kiisimu huonekana katika, mijarabu na jarabati ya mwisho wa muhula. Vilevile inaonekana katika uzungumzaji wa mwanafunzi anapowasilisha mbele ya wenzake. Wahadhiri wameeleza kuwa mabadiliko haya yanaonekana katika maandishi ya mitihani. Kutokana na jinsi wanavyopanga na kueleza hoja katika mitihani hii inaonesha kuimarika au kudorora kwa umilisi wa kiisimu. Matokeo yameonesha kuwa wahadhiri wanaweza kukadiria umilisi wa wanafunzi katika mazungumzo kupitia vigezo vya kusitasita, kushindwa kujibu maswali, kurudiarudia maneno, kucheka, kunyamaza, matamshi mabaya ya maneno, kiimbo kibaya, kuchanganya na kuhamisha misimbo, kutofuata ruwaza maalumu na ung'amuaji wa maana ya maneno. Wanafunzi wanaoyaonesha haya inasemekana kuwa wana umilisi wa kiwango cha chini. Kwa ujumla vigezo vitatu muhimu vinatumiwa kuonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu. Vigezo hivi ni katika mazungumzo, maandishi na usomaji.

Mahitimisho kulingana na madhumuni

Utafiti huu umechunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kimataifa metropolitan na changamoto ambazo wanafunzi na wahadhiri hupitia wakati wa kusoma na kufundisha isimu katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na matokeo haya wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanaonesha umilisi wa kiwango cha chini ikilinganishwa na wale wa mwaka wa nne. Umilisiwao umeonekana kuimarika wakati wanafunzi wanapoendelea kusoma. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa wanafunzi wanapofika mwaka wa nne kuna wale ambao huwa wameimarika katika lugha ya Kiswahili na kulikuwa na wale ambao wanakuwa na umilisi wa chini kama inavyoonekana katika jarabati ya mwaka wa nne. Wale wanaoimarika wametoa sababu kuwa wanapenda lugha hii na wana motisha ya kusoma kwa bidii, kwa sababu wanajua kile wana- weza kupata baada ya kumaliza masomo yao. Utafiti umeeleza kuwa vipengee vinavyotumika katika kupima umilisi wa kiisimu vilikuwana upungufu wake kama ilivyojadiliwa hapo mbeleni ingawa ndivyo vinavyotumiwa na wa- hadhiri. Vipengee hivi vimeonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswa- hili. Kwa mfano jarabati maandishi ni rahisi kupima umilisi wa kiisimu kuliko jarabati ma- zungumzo. Kutokana na nadharia ya Lehmann kuhusu umilisi wa kiisimu na ile ya Gardner ya mielekeo kuhusu lugha ya pili, imebainika kuwa wanafunzi wa kike wana umilisi wa ki- wango cha juu kuliko wenzao wa kiume. Hali hii inatokana na mielekeo yao chanya. Wana- funzi wa kiume wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

Kiswahili. Ili kuboresha uandikaji wa isimu na kuboresha matokeo ya mtihani wa Kiswahili, yatakikana makosa haya yarekebisha- we. Kurekebisha makosa ya kisarufi kunahitaji mbinu mwafaka ambazo ni wazi kwa wana- fuzi na wahadhiri. Kulingana na madhumuni ya kwanza ya utafiti huu kuhusu viwango vya umilisi wa kiisimu, utafiti unatoa mapendekezo yafuatayo;

- (i) Stadi za lugha ya Kiswahili zikiwa ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika zis- hughulikiwe ipasavyo ili kuweza kupima viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Uganda.
- (ii) Marekebisha ya makosa ya kisarufi yatakayobainishwa katika kazi za wanafunzi yaelewe wanafunzi darasani.
- (iii) Vipengee vinavyoonyesha mabadliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha vya paswakueleza kwa wanafunzi ili waelewe na kuvitumia katika maandishi na mazungumzo yao.
- (iv) Wanafunzi wanaofanya vizuri wapewe motisha ya aina yoyote ili kuzidi kuwapa msukumo wa kufanya vizuri zaidi. Aidha, wanafunzi ambao utendaji wao si mzuri, waweze kusaidiwa ili waimarika katika umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Vipengee vinavyoonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ni vingi. Hata mwanafunzi ambaye ataonesha kusitasita katika mazungumzo, kuchanganya na ku- hamisha msimbo, matamshi mabaya ya maneno, kiimbo kibaya na kutokuwa na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili huonesha kuwa umilisi wake ni wa kiwango cha chini katika lugha husika. Wahadhiri wamebaini kuwa, wao hujua kuwa mwanafunzi ameimarika kupitia mjarabu na jarabati ya mwisho wa muhula. Vilevile wanaweza kuchun- guza jinsi wanavyowasilisha kazi zao katika mihadhara mbele ya wenzao. Wahadhiri wana- weza kukadiria kuimarika kwao. Utafiti unapendekeza kuwa vigezo vingine vitafutwe vya kuelezea badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha Kiswahili.

MAREJELEO

Adams, D. (1993) Defining education quality, University of Pittsburg: USA

Alreck, L. & Settle, R. (1995). Survey Research handbook. Chicago: Irwin publishers.

Al – Juboury, N (1999). A Language Teacher's Guide to Assessment, Iraq: University of Baghdad.

Baker, C. (1992). Altitudes and Language. Clevedon: Multilingual Matters.

Babusa, H. (2010). Uchanganuzi linganzu wa mielekeo na umilisi wa wanafunzi wa Kiswahili katika mkoa wa Nairobi na Pwani: PhD Thesis ambayo haijchapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

Buliba, L. (1998). Utata katika istilahi za isimu ya Kiswahili. Makala ambayo hayajachapishwa, yaliyowasilishwa katika kongamano la Kiswahili, Kenyatta University, 23-25 Septemba 1998.

Chomsky, N. (1986). Knowledge of language, its nature and use. Cambridge: Mass MIT press.

Edwards, J. (1982). Language attitudes and their implications among English speakers. London: Edward Arnold.

Ellis, R. (2004). The definition of L2 explicit knowledge. Language learning.

Essa, R. (2001) Evaluation of oral efficiency of intermediate school teachers of English. Unpubl. MA Thesis, University of Al Mustansiriyah, college of Teachers.

Fasold, R. (1984). Sociolinguistics of Society. Blackwell Publishers, USA:

Flutcher, G. & F. Davidson. (2007). Language Testing and Assessment: An Advance Resource Book. New York, Routledge Taylor.

Flick, U. (1998). An Introduction to Qualitative Research. London: Sage.

Fillmore & Charles, J. (1979). Individual differences in language ability and language Behavior. New York: Academic press

Fraser, B. & Nolan, W. (1981) "The association of deference with linguistic forms". International Journal of Sociology of Language 27: 93-100.

Friedrich, P. (2000). English in Brazil: function and attitudes. World Englishes.

Furaha, J. (1991). Matumizi ya Lugha mjini Malindi: Jinsi Mielekeo inavyoathiri Uteuzi wa Lugha. Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Kenyatta

Gardner, R.C. (1985). Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitude and Motivation. London: Edward Arnold.

Gardner, R. & Smythe, P. C. (1981). On the development of the Attitude/Motivation Test Battery. Canadian Modern Language Review.

Gachiri, O. (2009) Kenyan Language Ideologies, Language Endangerment an Gikuyu (Kikuyu): How Discourses of Nationalism, Education and Development have

Received: 17.04.2024

Accepted: 23.04.2024

Published on: 29.04.2024

Gorman, T. (1974). The Teaching of Languages at Secondary Level, katika: Whitely, W.H. Language in Kenya. Nairobi: OUP.

Habwe & Karanja (2004). Misingi ya sarufi ya Kiswahili. Nairobi. Phoenix publ.

Halloran, J. (1967). Attitude Formation and Change. Great Britain: Leicester University Press.

Hoffman, (1977). Empathy prosocial: Its development and application in Keasey, Nebraska symposium on motivation; vol 25 (169-218).

Models and Methods. London & New York: Academic Press.

Jokey, M. (2007). An assessment of intermediate school Teachers English classroom, Unpul MA. Thesis. University of Baghdad.

Landweer. (2000), Indicators of Ethno Linguistic Vitality'. Notes on Sociolinguistics

Kombo, D. & Tromp, A. (2006). Propasal and thesis writing: An introduction; Nairobi: Pauline publications Africa.

Kitsao, R (2015) Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika kata ya Ganze, Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa: Pwani University.

Macaro, L, (2003) Teaching and learning a second language. A review of recent research. London: Bookcraft Ltd.

Malhotra, K. & Birks, S. (2007). Marketing Research: An applied approach. London: Prentice Hall.

Munialo (2009) Mielekeo ya wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shule za msingi wilaya Nyando. MA thesis haijachapishwa: Moi University.

Mutungu, (2001) Makosa ya Kileksia katika Insha za Wanafunzi wa Kidato cha kwanza. Tasnifu ya M.A. (UON)

Mwangi, B (2014). Umilisi wa stadi za maamkizi katika ujifunzaji wa Kiswahili. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ng'ong'a, O (2002). An assessment of University English language teacher Education in the light of classroom needs. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa: Kyambogo University.

Onyango, P. (1998). Jinsi ya kuimarisha kozi za Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Uganda . Makala ambayo hayajachapishwa ambayo yaliwasilishwa katika kongamano la Kiswahili lililokuwepo tarehe 23-25 Septemba, 1998, Kenyatta University.

Ramadhan. K. (1998). Assessing the proficiency competence of primary school teachers of English in Baghdad. Unpul. MA. Thesis. University of Baghdad.

Raheem. H. (2003) Oral profficiency of primary school teachers in English in Iraq. Unpul. MA. Thesis. An Arabic Higher institute of Education and Psychology Studies.

Savignon, N. (1983). Communicative competence, theory and practice. New York: Mcgraw

Tan, R. (1994). The use of English in selected domains amongst first year students of the Faculty of Arts and Social sciences in the University of Malaya. Unpublished M.A. thesis. University Malaya, Malaysia.

Verma, S. (1997). Modern Linguistics, An introduction. New Delhi: Oxford University Press.

Walliman, N (2011), Reseach Methods; The Basic, London & New York; Routledge Taylor & Francis Group

Wanyoike, P. (1978), Vikwazo katika mafunzo ya Kiswahili Kenya. Lugha 5-3

Weiner, S (2000), Perception of word likeness: Effects of segment probability, London: CUP.

Wendo, N. (2009), Language Policy in Kenya: Negotiation with Hegemony “ The Journal of Pan African Studies, vol.3, no.1. pp 121 - 138

White, L. (1959). Motivation considered the concept of competence. NewYork: Rockvillepike

Widdowson, Henry G. (1973). An applied linguistic approach to discourse analysis (Un published PhD dissertation). Edinburgh: University of Edinburgh.

Woods, D. (1995). Attitudes towards French, national Languages, and mother tongues across age and sex in Congo. New Jersey: African World Press,